

KURUDI KWENYE MAJENGO YA SHULE

Nini cha kujua kuhusu kusoma kwa kuchanganya

Shule za umma za Salem-Keizer kwasasa ziko kwenye mpito wa kupanga kusoma kwa kuchanganya kuanzia Marchi kwa wanafunzi wa chekechea mpaka darasa la 1, madarasa mengine yatafuata wiki inayofuatia. Katika kusoma kwa kuchanganya, wanafunzi watakuwa wanasoma siku mbili shuleni na kuhudhuria masomo ya mtandao siku mbili kwa wiki. Afya na usalama ni kitu cha kipaumbele katika wilaya wakati tunaporudi kusoma uso kwa uso.

**Kuanzia
mwezi
Septemba**

KUONGEZEKA KWA ITAKADI YA USALAMA KUHUSU COVID-19

Itikadi ya usalama kuhusu COVID-19 imekuwa ikitumika ndani ya majengo kuanzia Septemba

- Kuongeza itikadi za usafi katika mashule na mabasi
- Mratibu wa umbali wa kimwili katika kila kituo
- Barakoa zinatakiwa kwa wanafunzi na wanafanyakazi

**Marchi
2**

KURUDI KATIKA MAJENGO YA SHULE: CHEKECHEA MPAKA DARASA LA 1/ PROGRAMU MAALUM KATIKA KUSOMA KWA KUCHANGANYA

Wiki ya kwanza kusoma kwa kuchanganya itakuwa kwa wanafunzi wa chekechea na darasa la kwanza itakuwa wiki ya Marchi 2. Wanafunzi watahudhuria masomo uso kwa uso siku ya Jumanne na Alhamisi au siku ya Jumatano na Ijumaa. Katika siku za mbadala, wanafunzi watahudhuria masomo kwa njia ya mtandao. Siku ya Jumatatu imewekwa kwa kuwafikia wanafunzi wanaohitaji msaada.

Wanafunzi ambao wanashiriki madarasa ya ngazi mbalimbali katika programu maalumu pia watakuwa kwenye mpito wa kusoma kwa kuchanganya Marchi 2. Hizi programu maalumu zinajumuisha vituo vya ukuaji wa kihemko (EGCs), Maendeleo ya chekechea, darasa la kwanza na pili, vituo vya maendeleo ya kujifunza (DLCs), Madarasa ya kujifunza ujuzi wa maisha (LSCs), Programu ya kuingilia mawasiliano ya kijamii (SCIP) na Vituo vya rasilimali kwenye elimu (ERCs).

**Marchi
9**

KURUDI KATIKA MAJENGO YA SHULE DARASA 2-3, KUSOMA KWA KUCHANGANYA

Lengo la wilaya ni darasa la pili na darasa la tatu kuanza kusoma kwa kuchanganya katika wiki ya Marchi 9

**Marchi
16**

KURUDI KATIKA MAJENGO YA SHULE DARASA LA 4 - 5

Lengo la wilaya ni darasa la nne na darasa la tano kuanza kusoma kwa kuchanganya katika wiki ya Marchi 16

KUPANULIWA KWA KUSOMA WATU WACHACHE

Wilaya itapanua kusoma kwa watu wachache haswa wale wa sekondari lakini muangalizo utakuwa wale walio mwaka wa mwisho kumaliza shule na wanahitaji msaada ili waweze kumaliza. Taarifa za ziada na mipango ya kuwarudisha wanafunzi wa sekondari kwenye majengo ya shule kwa ajili ya kusoma kwa kuchanganya itatolewa wiki zinazokuja.

MASWALI KUHUSU KUSOMA KWA KUCHANGANYA?

Tuma maswali yako. Hatutaweza kujibu kila mtu na maswali yake; Hata hivyo, majibu yatawasaidia wakuu wa shule za msingi kuandaa taarifa kwa wazazi.

<http://bit.ly/K5-inperson>

